

MPISHI WA WANA

T. S. Y. Sengo

1. Kilaji kuwa chakula, cha muhitaji mpika
Si cha kuku cha jalala, panya kilaji cha paka
Kuamka si kulala, kula si kama kupika
Mpishi wa wana, andaa turithi

2. Baadhi wanazo ila, mchele kuubambika
Wengine wana aula, rangi zao kuzipaka
Na wapishi wana ala, za makosa kuepuka
Mpishi wa wana, andaa turithi

3. Hu mpishi mwenye hila, pilau kukakauka
Pilipili kujazila, machoni kumwekamweka
Bali wana wandikila, malaji ya kusifika
Mpishi wa wana, andaa turithi

4. Mbele yetu kuna jola, si la chini kutandika
Vizuri ukililola, linafaa kugawika
Zuti kwa ndoa na sola, maisha kuhifadhika
Mpishi wa wana, andaa turithi

5. Usitupikie pulla, mafuta kutononoka
Usitupeleke kwala, ngomani kurukaruka
Bali twataka pahala, mipaka kuhifadhika
Mpishi wa wana, andaa turithi

6. Kumbuka kalla Taala, ya haki kutimizika
Mbuzi kondoo na swala, wape mundu na mashoka
Mbele sharuti kuola, dhuluma kuzilika
Mpishi wa wana, andaa turithi